



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 6, Issue 1, 2023

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama

Vince Arasa Nyabunga^{1*} Dkt. Miriam Osore, PhD¹ na Dkt. Leonard Chacha Mwita, PhD¹

¹ Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100, Nairobi, Kenya.

* ORCID ID: <https://orcid.org/0000-0003-3199-7707>; Barua pepe ya mawasiliano: vincenyabunga21@gmail.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1036>

Tarehe ya Uchapishaji: IKISIRI

04 Januari 2023

Istilahi Muhimu:

*Hali ya Maisha,
Uinjilisti,
Skopos.*

Tafsiri imekuwa njia ya kuhamisha maarifa na ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine kwa muda mrefu lakini imetambuliwa kama taaluma ya kiusomi siyo miaka mingi iliyopita (Munday, 2001). Tafsiri zilizopo zimefanywa kwa kuzingatia mtazamo wa ulinganifu wa visawe vya lugha chanzi na lugha pokezi bila kuhusisha dhana ya uelewaji na ufasiri wa hadhira lengwa. Utafiti huu ulivuka mtazamo huo na kuchunguza uelewaji na ufasiri wa mafunzo tafsiri katika Njia Salama. Matini za kidini hutumiwa katika maeneo ya maabadi ili kuadilisha, kukuza mahusiano na kutangamanisha jamii. Vilevile, huwasilisha mafunzo muhimu ya kihistoria ya kidini ambayo yanafaa kueleweka na kufasirika kwa njia ya wazi. Hata hivyo, uchanganuzi wa awali wa matini tafsiri, unaonyesha kuwepo kwa matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe wa hali ya maisha na uinjilisti. Kwa hivyo, lengo la utafiti huu ni kuthamini mafunzo hayo na kubainisha namna matatizo hayo yanavyojitokeza. Hali kadhalika, utafiti huu unakusudia kuthibitisha iwapo matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe katika matini teule yanasababishwa na tofauti za kiisimu, kimtindo, kimuundo na kitamaduni baina ya lugha asilia na lugha pokezi. Katika kutekeleza jukumu hili, washiriki 140 walishirikishwa kutoa data ya utafiti. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo na kitakwimu. Kwa hivyo, viongozi 42 na waumini 98 kutoka kanisa saba teule walishiriki. Washiriki waliojua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili walisailiwa na kuhojiwa. Nadharia ya skopos inayoweka mkazo kwenye matini tafsiri iliongoza utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalilenga kuchangia uelewaji na ufasiri wa ujumbe katika matini tafsiri za kidini.

APA CITATION

Nyabunga, V. A., Osore, M & Mwita, L. C. (2023). Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), 1-15. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1036>.

CHICAGO CITATION

Nyabunga, Vince Arasa, Miriam Osore and Leonard Chacha Mwita. 2023. "Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 1-15. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1036>.

HARVARD CITATION

Nyabunga, V. A., Osore, M & Mwita, L. C. (2023) "Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 1-15. doi: 10.37284/jammk.6.1.1036.

IEEE CITATION

V. A. Nyabunga, M. Osore, & L. C. Mwita "Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 1-15, Jan. 2023.

MLA CITATION

Nyabunga, Vince Arasa, Miriam Osore & Leonard Chacha Mwita. "Kutathmini Mafunzo Tafsiri katika Matini za Kidini: Mfano wa Njia Salama". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Jan. 2023, pp. 1-15, doi:10.37284/jammk.6.1.1036.

UTANGULIZI

Tafsiri imekuwa njia ya kuhamisha maarifa na ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine kwa muda mrefu lakini imetambuliwa kama taaluma ya kiusomi siyo miaka mingi iliyopita (Munday, 2001). Tafsiri zilizopo zimefanywa kwa kuzingatia mitazamo anuwai ya kiuchunguzi kama vile umatini, makosa ya kitafsiri na ulinganifu wa visawe vya lugha chanzi na lugha pokezi bila kuhusisha dhana ya uelewaji wa ujumbe katika matini tafsiri (Venuti, 2008). Utafiti huu ulilenga kuvuka na kuchunguza uelewaji na ufasiri wa mafunzo tafsiri katika *Njia Salama* iliyoandikwa na White ili kubainisha namna ujumbe tafsiri wa hali ya maisha na uinjilisti ulivyohamishwa kutoka matini asilia hadi makala pokezi.

Nida na Taber (1969) wanasema kuwa mtafsiri ana jukumu la kuwakilisha maana ya lugha chanzi katika lugha pokezi kwa njia ya wazi na kutumia miundo ya lugha inayokubalika. Kwa mujibu wao, mtafsiri anafaa ajieleze wazi huku akiheshimu sifa na miundo ya lugha inayohusika katika tafsiri. Hata hivyo, mapitio ya awali yalibainisha kuwa kitabu tafsiri cha *Njia Salama*, kina mafundisho tatanishi yanayohusiana na uelewaji na ufasiri wa ujumbe. Hali kadhalika, yanavyosomwa, kufahamika na kufasiriwa kwa njia tofauti miongoni mwa waumini wa SDA. Kwa mujibu wa Knight (2009), dhehebu SDA limeenea katika pembe zote za bara saba za ulimwengu: Afrika, Asia, Uropa, Australia, Antarctica, Marekani Kusini na Kaskazini. Kanisa la SDA tangu mwanzo wake, limeendelea kushuhudia mabadiliko mengi katika mafundisho yake kama vile unabii, hali ya kimaisha na uinjilisti,

masuala ambayo utafiti huu unalenga kuchunguza. MSINGI WA NADHARIA

Utathmini wa matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe katika *Njia Salama* utaongozwa na nadharia ya *Skopos*. Nadharia hii iliasisiwa na Vermeer (1978). Neno *skopos* linatokana na neno la Kigiriki lenye maana "nia ya kutafsiri". Nadharia hii huchukulia shughuli ya kutafsiri kama kitendo kilicho na malengo. Kitendo hicho kinafaa kumlenga mpokeaji katika utamaduni na mazingira ya msomaji. Kwa mujibu wa nadharia hii, kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa, kwa kuzingatia lengo, mpokezi na mazingira lengwa (Schaffner, 1998).

Kulingana na Vermeer (1989), hakuna matini chanzi iliyo na tafsiri moja tu ambayo ni sahihi na inayokubalika. Hivyo basi, kila tafsiri lazima itangaze skopos yake, yaani ieleze nia yake. *Skopos* ya matini lengwa si lazima ifanane na *skopos* ya matini chanzi. Kwa hivyo, inabidi *skopos* ya matini lengwa ifanuliwe ili tafsiri itekelezwe kwa ufanisi.

Mihimili ya *skopos* ni muhimu katika utafiti huu kwa njia nyingi. Inaweka mkazo kwenye matini lengwa. Reiss (1990) anaounga mkono nadharia hii kwa kusisitiza kuwa, mara tu mtu anapojua nia ya tafsiri, mikakati mingine kama vile urekebishaji na uundaji upya wa matini utajitokeza wenyewe wakati wa kutafsiri. Kwa hivyo, licha ya hayo, matini tafsiri haibainishwi tu na matini chanzi bali pia hubainishwa na nia ya kutafsiri.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulilenga washiriki 4010 wa dhehebu la SDA. Kwa hivyo, sampuli tarajiwa ya utafiti

ilikuwa washiriki 140, yaani viongozi 42 na waumini 98 katika makanisa saba yatakayoteuliwa kwa kutumia fomula ya Kothari (2004) ili kuteua ukubwa wa sampuli:

$$n = \frac{Z^2 pq N}{e^2(N-1) + Z^2 pq}$$

$$p = 0.5, q = 0.5, Z = 1.96, e = 0.1$$

Maana ya viashiria: e = kosa tarajiwa (*error*), n = ukubwa wa sampuli, N = idadi ya washiriki wote, p = uwezekano kwamba kila mshiriki anayehusishwa ana ujumbe unaochunguzwa, q = uwezekano kwamba kila mshiriki anayehusishwa hana ujumbe unaochunguzwa.

$$n = \frac{1.96^2 * 0.5 * 0.5 * 4010}{0.1^2 * (4010 - 1) + 1.96^2 * 0.5 * 0.5} = 97$$

Ugawanaji wa sampuli ulikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali 1: Ukubwa wa Sampuli

Mji	Kongamano	Makanisa (Kiswahili)	Kanisa teuliwa	Wachungaji	Wahubiri	Walimu	Mashemasi
Eldoret	WKC	2	1	1	1	2	2
Kitale	NWKC	2	1	1	1	2	2
Kisumu	CNC	2	1	1	1	2	2
Homabay	KLF	2	1	1	1	2	2
Ranen	RC	2	1	1	1	2	2
Kisii	SKC	2	1	1	1	2	2
Nyamira	NC	2	1	1	1	2	2
Jumla		14	7	7	7	14	14

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Vilevile, ukubwa wa sampuli ya waumini kutoka makanisa shirikishi saba ya *Western Kenya Union Conference* (WKUC) ilikuwa kama ilivyoorodheshwa:

Jedwali 2: Ukubwa wa Sampuli ya Waumini

Kanisa	Mji	Kongamano	Waumini (Rejesta)	Waumini
Kisumu South SDA	Kisumu	CNC	600	15
Kibomet SDA	Kitale	NWKC	400	10
Manyatta SDA	Ranen	RC	560	14
Central SDA	Edoret	WKC	700	17
Owiro SDA	Homabay	KLF	450	11
Nyanchwa SDA	Kisii	SKC	800	19
Central SDA	Nyamira	NC	500	12
Jumla			4,010	98

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Njia za kukusanyia data zilikuwa hojaji, mahojiano na uchanganuzi wa matini. Mtafiti alitumia hojaji katika ukusanyaji wa data kwa sababu utafiti huu una vigezovigeu (*variables*) ambavyo havitaweza kuelezeka kwa njia ya moja kwa moja. Baadhi ya vigezovigeu hivyo ni pamoja na maoni, hisia na misimamo ya washiriki wa utafiti huu. Data ya aina hiyo inafaa kukusanywa kupitia hojaji (Touliatos & Campton, 1988). Waumini 98 walipewa hojaji kujaza na kujibu maswali yalikuwa funge na wazi.

Mahojiano ya utafiti huu yalikuwa funge. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), mahojiano funge, kila mshiriki anaulizwa aina fulani ya maswali yanayofanana. Mahojiano hayo yalikuwa ya kina zaidi na yalihatiji ujuzi na umakinifu wa mtafiti katika kuwaongoza wahojiwa ili kutoa taarifa zilizohitajika.

Mwisho, njia ya uchanganuzi matini ilitumiwa. Njia hiyo ilikuwa bora kwa kuwa ilimpa mtafiti nafasi ya

kufahamu uasilia wa lugha katika matini tafsiri, kupata data kwa wakati unaofaa, habari isiyoweza kuathiri utafiti na bila kupoteza muda. Kwa hivyo, mbinu ya uchanganuzi matini iliwezesha kuyatambua na kuyateua mafunzo katika *Njia Salama* cha White.

MATOKEO YA UTAFITI

Matokeo katika utathmini wa mafunzo tafsiri ya kidini katika *Njia Salama* yaliwasilishwa kwa awamu mbili: hali ya maisha na uinjilisti.

Jedwali 3: Uelewa na Ufasiri wa Hali ya Maisha

	Utukiaji	%
Maisha anayoishi mwanadamu ni ubatili	22	22.0
Kula lishe bora na kuvaa mavazi kadirifu	46	46.0
Ngumu na inahitaji uvumilivu na kumtegemea Mungu	18	18.0
Bila majibu	13	13.0
Jumla	99	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika *Jedwali 3*, waumini walitoa majibu na maoni tofauti kuhusu dhana ya *hali ya maisha*. Kwa mfano, walisema kuwa maisha ni ubatili (22%), kula lishe bora na ukadirifu wa mavazi (46%), maisha ni magumu na yanahitaji uvumilivu na kumtegemea Mungu (18%) na wengine hawakutoa majibu (13%). Kutokana na majibu ya wasailiwa, dhana ya hali ya maisha inaeleweka na kufasirika kwa njia tofauti miongoni mwa wanasabato. Kwa mfano, tazama funzo la *Upendo wa Mungu kwa mwanadamu* (*Njia Salama*, uk 1), linavyotafsiriwa katika mfano ufuatao:

Mfano wa 1

MA: Nature and revelation alike testify of God's love. Our Father in heaven is the source of life, of wisdom, and of joy. Look at the wonderful and beautiful things of nature. Think of their marvellous adaptation to the needs and happiness, not only of man, but of all living creatures... It is God who supplies the daily needs of all His creatures.

MP: Viumbe vya ulimwengu na jinsi Mungu alivyowafunulia wanadamu mambo yajayo, vyote huonyesha upendo wake Mungu. Baba yetu aliye mbinguni ndiye asili ya uhai, hekima,

Hali ya Maisha katika *Njia Salama*

White, katika matini ya *Njia Salama* anafundisha hali ya maisha kwa kupitia hatua kumi na tatu za kuongoza maisha ya Mkristo. Hatua hizo ni pamoja na upendo, haja ya mwenye dhambi kumhitaji Kristo, kutubu, kukiri, kutakazwa, imani na ukubalifu, maisha na kazi, kumfahamu Mungu, manufaa ya maombi, namna ya kushughulikia mashaka na kufurahia maisha katika Yesu (*Njia Salama*, Uk. 1-90). Wanasabato waliposailiwa kuhusu suala la hali ya maisha walitoa majibu na maoni kama inavyojitokeza:

na furaha... Mungu ndiye anayeviruzuku viumbe vyake vyote mahitaji yao ya kila siku.

Katika mfano wa 1 (i) funzo la upendo limetafsiriwa kama ifuatavyo: *Viumbe vya ulimwengu na jinsi Mungu alivyowafunulia wanadamu mambo yajayo, vyote huonyesha upendo wake Mungu*. Katika tafsiri hiyo, ujumbe katika vishazi vingine umepanuliwa. Kwa mfano, *Nature and revelation alike testify of God's love* chenye maneno (8) kimetafsiriwa kwa maneno mengi (15). Tatizo lingine katika mfano huo ni kuwa, mtafsiri amekosa visawe vya baadhi ya maneno. Neno *Nature* halina *kisawe* chake katika Kiswahili hali ambayo ilimlazimu mtafsiri kulitafsiri kama *viumbe vya ulimwengu*. Katika uhamishwaji huo, mtafsiri hajataja aina ya viumbe vya ulimwengu kwa kuwa kina vya kuonekana na visivyoonekana. Hali kadhalika, kuna baadhi ya vishazi ambavyo havijahamishwa. Kwa mfano kishazi *Look at the wonderful and beautiful things of nature* hakijatafsiriwa. Kwa hivyo, uhamishwa wa aina hii unawanyima wasomaji uasilia, uaminifu na ukubalifu kama vile nadharia ya skopos inavyofafanua (Reiss na Vermeer, 1984).

Pendo (2017), anasema kuwa tafsiri fafanuzi inayeyusha maana msingi katika kuhamisha ujumbe kutoka MA hadi MP. Naye Matamala (2009)

anamuunga mkono kwa kusema kuwa ukosefu wa visawe katika lugha lengwa humlazimisha mtafsiri kuunda maneno mapya, kutumia tafsiri elezi, utohoji na kadhalika. Hali hiyo inaweza kuongeza vipengele vingine vya lugha ambavyo havikuwa katika MA na kwa hiyo kuathiri uhamishwaji wa maana kutoka MA hadi MP. Tazama mfano:

(ii)

MA: *The apostle says, “Confess your faults one to another and pray one for another, that ye may be healed.” James 5:16.* (Steps to Christ, pg. 23).

MP: *Mtume Yakobo asema, “Ungameni makosa yenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpata kuponywa,” Yak.5:16.* (Njia Salama, uk2).

Katika mfano wa 1(ii) White alifunza funzo la kuungama dhambi zake (Njia Salama, uk.23-26); kwa njia ya kufanya maombi ya kweli, kukiri makosa na Wakristo kuombeana. Ilikuwa utamaduni wa enzi ya White Wakristo kuweza kukiri makosa yao hadharani bila kuwa na uoga au fedheha kwa sababu imani yao ilikuwa thabiti. Kwa hivyo, matokeo yalionyesha kuwa uhamishwaji wa utamaduni ulifanywa bila kuzingatia tofauti za kitamaduni baina ya jamii mbili husika. Waumini wa leo hawawezi kuungama dhambi hadharani kama enzi ya White. Basi, uhamishwaji huo unafaa kufanywa kwa malengo kwa mujibu wa nadharia ya *skopos*.

Kuhusu funzo la uaminifu na ukubalifu wa Mkristo (Njia Salama, uk. 32-37), White alifundisha wanasabato kuwa wanafaa kupata msamaha wa kutoka mbinguni ili apate ukubalifu. Tazama namna ujumbe huo ulivyowasilishwa katika mfano:

MA: *It is peace that you need..heaven’s forgiveness and peace and love in the soul.*

Money cannot buy it, intellect cannot procure it, wisdom cannot attain it; you can never hope, by your own effort, to secure it. But God offers it to you as a gift, “without money and without price.” (Isaiah 55:1).

MP: *Hali hii haiwezi kununuliwa kwa fedha, pia haipatikani kwa ajili ya akili wala elimu; tena huwezi kutumaini kuwa katika hali hiyo kwa juhudi zako mwenyewe. Bali utaipata bure mkononi mwa Mungu kama karama yake, “pasipo fedha na pasipo thamani.” Isa.55:1.*

Katika mfano wa 1(iii) funzo la uaminifu na ukubalifu wa Mkristo lilitafsiriwa kwa njia ifuatayo: Kwa mfano, vishazi *It is peace that you need...; heaven’s forgiveness and peace and love in the soul* havijahamishwa kutoka MA hadi MP. Hii ni sehemu muhimu katika ujumbe huu lakini haipatikani katika MP. Aidha kuna vipashio vingine ambavyo vimeongezwa kwenye MP. Kwa mfano, maneno kama *wala elimu* na *utaipata bure* yameongezwa katika MT. Kwa hivyo, matokeo ya tafsiri hiyo yalionyesha kuwa tofauti na iliwanyima wasomaji uelewa na ufasiri wa ujumbe uliosawa baina ya matini asilia na makala pokezi.

Brooke (2011) anafafanua kuwa ilikuwa utamaduni wa Wakristo wa zamani kufuata maadili ya kikanisa ikilinganishwa na nyakati za leo. Anaendelea kusema, “Maadili ya kikanisa yanategemea mtu binafsi; ukweli wako ni wako na wala si wangu. Haki yako si lazima iwe haki yangu.” Filosofa ya aina hii imeenea kwa mapana katika jamii nyingi za Kikristo. Matokeo yalionyesha kuwa Wakristo wa siku hizi wanaabudu mali na pesa na kwa hivyo mahubiri kama hayo hayatapewa uzito unaostahili.

Mashemasi nao walisailiwa kuhusu mafunzo ya uaminifu na ukubalifu kama sehemu ya hali ya maisha. Tazama matokeo:

Jedwali 4: Mashemasi kuhusu Hali ya Maisha

	Utukiaji	%
Viwango vya maadili vimezorota kanisani	3	37.5
Wanasabato wanafuata maadili ya kikanisa	4	50.0
Wanasabato wanaofuata mafundisho ya White wanatengwa na wanasabato wengine wasiofuata ujumbe huo	1	12.5
Jumla	8	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika *Jedwali 4*, mashemasi wakubaliana kuwa viwango vya uaminifu na ukubalifu vimezorota kanisani (37.5%), idadi kubwa ya waumini inafuata maadili ya kikanisa (50%) na (12.5%), inatengwa kwa sababu ya mafundisho ya White. Kutokana na matokeo hayo, ni wazi kuwa (50%) ya washiriki, wanathibitisha kuwa uaminifu na ukubalifu miongoni mwa wanasabato una changamoto za uelewaji na ufasiri kanisani.

Kuhusu mafunzo ya mahusiano ya kushirikiana kanisani katika *Njia Salama* (uk. 71). Mtafsiri aliamisha ujumbe huo kwa njia tatanishi. Tazama mfano:

MA: We sustain a loss when we neglect the privilege of associating together to strengthen and encourage one another in the service of God.

MP: Tunaona upungufu kama tunakosa kushirikiana na wengine kwa kujiimarisha

Jedwali 5: Mahusiano Kanisani

	Utukiaji	%
Hakuna upendo na amani kanisani	3	42.9
Mapendeleo katika kutoa nyadhifa kwa washiriki kanisani	3	42.9
Tofauti za kiuchumi na kitabaka kanisani	1	14.3
Jumla	7	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika *Jedwali 5*, wahubiri walitoa sababu za kuzorota kwa mahusiano kanisani kama ifuatavyo: hakuna upendo na amani kanisani (42.9%), hakuna haki katika kutoa nyadhifa kanisani (42.9%), mahusiano yamesambaratika kwa sababu ya tofauti za kiuchumi na matabaka kanisani (14.3%). Matokeo hayo yanaonyesha kuwa hali ya maisha ya mwanasabato imebadilika kwa sababu za kibinafsi, kijamii na kuzuka kwa matabaka kanisani. Matokeo hayo, vilevile, yalionyesha kuwa waumini hawajaelewa na kufasiri vyema mafunzo ya White kuhusu udumishaji wa uhusiano mwema kanisani.

Katika (uk. 56), White alifundisha namna ya kumjua Mungu. Alifundisha kuwa kuna njia nyingi Mungu anazitumia kujijulisha kwa waumini. Tazama mfano:

mioyo yetu wenyewe kwa wenyewe katika kumtumikia Mungu.

Katika mfano wa 1 (iv) mtafsiri aliamisha ujumbe kwa njia ifuatavyo. Kwa mfano, sentensi *We sustain a loss when we neglect the privilege of associating together* imetafsiriwa kama *tunaona upungufu kama tunakosa kushirikiana na wengine*. Katika tafsiri hiyo, *we sustain a loss* maana yake si *tunaona upungufu* kama ilivyotafsiriwa. Maana yake sahihi ingekuwa *tunajutia au tunapata hasara*. Vilevile, maana ya *encourage one another* imeondolewa katika MP. Tafsiri yake ingekuwa kuhimizana mmoja na mwingine. Kwa hivyo, matokeo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe huo unakanganya wasomaji kwa sababu ya utata unaosababishwa na vipashio vya kiisimu.

Kuhusu mafunzo ya uhusiano mwema kanisani, wahubiri walihojiwa na walitoa maoni kama inavyojitokeza katika mfano:

MA: The open heart will be impressed with the love and glory of God as revealed through the works of His hands.

MP: Moyo unaofunuliwa utaona upendo na utukufu wa Mungu jinsi unavyoonekana katika matendo yake na katika kazi za mikono yake.

Katika mfano wa 1 (v) mtafsiri aliamisha ujumbe kwa njia ifuatavyo. Kwa mfano, ujumbe katika usemi *the open heart* umetafsiriwa kama *moyo unaofunuliwa* badala ya *moyo mkunjufu* au *moyo mkarimu*. Kirai *will be impressed with the love and glory of God* kimetafsiriwa kama *utaona upendo na utukufu wa Mungu* badala ya *utafurahishwa na upendo na utukufu wa Mungu*. Vilevile, kishazi *as revealed through the works of His hands* kimetafsiriwa kama *jinsi unavyoonekana katika matendo yake na katika kazi za mikono yake*. Katika kishazi hicho, mtafsiri ameongeza maana ya

matendo yake ambayo haikuwepo katika matini asilia. Kwa hivyo, matokeo yanadhihirisha kwamba mtafsiri hakuzingatia vipengele vya uaminifu na ukubalifu katika kuhamisha ujumbe wake hali ambayo inaathiri uelewaji na ufasiri wa msomaji.

Mazzalongo (2019), anaeleza dhana ya hali maisha kama hali ya Mkristo kupata mwamko mpya, kuathiriwa na mafunzo ya Kristo kwa njia mpya. Amebainisha sifa saba za Mkristo: kuamini Mungu, kujitambulisha na dini, kusoma Biblia, uokovu, kuhudhuria kanisa na kuzingatia maisha ya Ukristo. Kwa hivyo, hali ya maisha, ni matamano, mielekeo, tabia na masuala mengine yanayotokana na watu, makundi, jamii au utamaduni unaojitokeza kama njia ya kuishi.

Jedwali 6: Dhana ya Uinjilisti

	Utukiaji	%
Mafundisho ya Neno la Mungu	8	8.1
Ni mwito kutoka kwa moyo	4	4.0
Kujitolea kufanya kazi ya Mungu kwa lolote lile	7	7.1
Sina ufahamu	1	1.0
Jinsi matukio fulani yatakavyokuwa wakati ujao	1	1.0
Mahubiri yanayofanywa kupitia uuzaji na ununuzi wa vitabu	3	3.0
Uenezaji wa Neno la Mungu	41	41.4
Bila majibu	34	34.3
Jumla	99	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika *Jedwali 6*, matokeo yalionyesha kuwa idadi kubwa ya waumini waliosailiwa inadhihirisha kuwa uinjilisti ni uenezi wa neno la Mungu (41.4%) na waumini (34.3 %) hawana ufahamu wa dhana ya uinjilisti. Kundi la waumini wasiofahamu dhana ya uinjilisti, inathibitisha kuwa kuna matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe katini matini teule.

Jedwali 7: Tafsiri za Anwani Katika Njia Salama

MA	MP	TY
<i>Steps to Christ</i>	<i>Njia Salama</i>	Hatua za Ukristo
God's Love For Man	Jinsi Mungu Anavyowapenda Wanadamu	Upendo wa Mungu kwa Mwanadamu
The Sinner's Need of Christ	Jinsi Mwenye Dhambi Anavyomhitaji Kristo	Mwenye Dhambi Kumhitaji Kristo
Repentance	Kutubu	Toba
Confession	Kuungama Dhambi	Kukiri Dhambi
Consecration	Kujitoa Kuwa Wa Mungu	Wakfu
Faith And Acceptance	Kumwamini Mungu Na Kukubaliwa Naye	Imani Na Ukubalifu

Matokeo ya Uinjilisti katika Njia Salama

Heck (2011), anaeleza dhana ya injili kuwa ni uenezaji wa habari ya Yesu. Mahubiri hayo yaliambatana na ujumbe wa kusameheana kwa Wakristo na namna ya kuishi maisha ya milele kupitia imani. White akinukuu kitabu cha Waefeso (4:12) kuwa uinjilisti ni miongoni mwa huduma kama vile utume, uhubiri, ualimu na unabii ambao wahudumu wake huteuliwa kwa utaratibu mahsusi. Lakini waumini waliposailiwa kuhusu uelewa na ufasiri wa uinjilisti walitoa maelezo yanayotofautiana kama ifuatavyo:

Tafsiri za Anwani

Katika kufunza uinjilisti, White alitumia anwani mbalimbali kama iliorodheshwa katika *Jedwali 6* hapa chini. Ingawa alifaulu katika uteuzi wa anwani hizo, mtafsiri alisababisha tafsiri finyu na pana ambayo iliathiri uelewaji na ufasiri wa sura zinahusika katika *Njia Salama*. Tazama mfano:

MA	MP	TY
The Test of Discipleship	Dalili Ya Kuwa Wanafunzi Wake Kristo	Majaribu Ya Ufuasi/Ukristo
Growing Up Into Christ	Haijatafsiriwa	-
The Work And The Life	Kazi Na Maisha, Jinsi Vinavyohusiana	Kazi Na Uzima
A Knowledge Of God	Kumjua Mungu	Maarifa Ya Mungu
The Privilege Of Prayer	Kuomba Ni Faradhi Yetu	Manufaa Ya Maombi
What To Do With Doubt	Yatupasayo kufanya tunapokuwa na Mashaka moyoni	Tufanye Nini Tukiwa Mashakani
Rejoicing In The Lord	Kufurahia Mungu	Kufurahia Katika Bwana

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Uhamishaji wa anwani na mada mbalimbali za sura kumi na tatu katika *Njia Salama* ni jambo ambalo limetatiza wasomaji lengwa. Mtafsiri alikosa visawe linganifu vya anwani na mada za lugha pokezi. Kwa mfano, *Steps to Christ* (MA) ilitafsiriwa kama *Njia Salama* (MP) badala ya

Hatua za Ukristo (TY). Katika makala asilia, anwani inazungumzia wingi wa hatua ambazo Mkristo anafaa kutimiza kabla kupata uokovu lakini inapohamishwa hadi MP, inaleta dhana ya umoja. Kuhusu dhana hii, waumini walitoa maoni:

Jedwali 8: Tafsiri ya 'Steps to Christ'

	Utukiaji	%
Hatua kwa Kristo	5	5.1
Njia na tabia zinazoaminika ili kufika mbinguni	6	6.1
Sina ufahamu	5	5.1
Ubatizo	1	1.0
Njia za kumfuata Kristo na maadili mema	43	43.4
Bila jibu	39	39.4
Jumla	99	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika *Jedwali 8*, matokeo yanaonyesha kuwa waumini zaidi ya (51%) hawakuelewa fasili ya dhana ya *Steps to Christ* ingawa wengine walitoa majibu yanayoelekea kuwa sahihi (48%) kama inavyojitokeza katika *Jedwali 6*. Hali kadhalika, kuna washiriki wengine hawakuelewa dhana hiyo (39.4%).

Vilevile, ukosefu wa visawe ulimfanya mtafsiri kusababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri katika kutafsiri anwani nyingi, hali ambayo pia inamnyima msomaji uasilia na maana msingi ya matini chanzi kama inavyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo.

Anwani nyingine iliyohamishwa kwa njia tatanishi ni *Consecration* (MA) iliyohamishwa kama *Kujitoka kwa Mungu*. Maana ya dhana hii katika LA kwa mujibu wa *Kamusi ya Cambridge* ni **utakatifu** unaotokana na wakfu maalumu. Pia ni utengwaji wa mali au mtu kwa ajili ya shughuli za dini lakini katika lugha pokezi, maana hiyo haijitokezi. Dhana

ya *Kujitoka kwa Mungu* inaleta maana tofauti katika makala pokezi. Utukufu ni shughuli ya kidini lakini katika matini pokezi *kujitoka kwa Mungu* ni kitendo cha mtu binafsi.

Matokeo ya uchanganuzi huo yalionyesha kuwa mtafsiri amefanya tafsiri aina mbili, *pana* na *finyu*. Tafsiri pana inarejelea urefushaji wa habari katika matini tafsiri kupita kiasi ya ile iliyokuwepo katika matini asilia. Nayo tafsiri finyu inarejelea pale ambapo matini lengwa ina habari chache kuliko ile iliyopo katika matini chanzi (Wang, 2012).

Kwa hivyo, ulinganishi wa anwani zilizotafsiriwa katoka Kiswahili hadi Kiingereza unaonyesha kwamba kuna changamoto za kupata visawe mwafaka. Hali hiyo, ilisababisha matatizo kama vile udondoshaji, upotoshaji, tafsiri finyu, tafsiri pana pamoja na matatizo ya kuchujusha nduni mahususi za matini hizo. Kwa mujibu wa Chaula (2012),

matatizo ya kutafsiri matini kwa upana na ufinyu yanasababishwa na sababu zifuatazo:

- a) Husababishwa na tofauti za kitamaduni,
b) kutokuwa na uwezo wa lugha ya mtafsiri, c) Ujuzi wa historia ya mtafsiri na uzoefu wake

Tafsiri za aina hii zinazosababisha na matatizo ya uelewaji na ufasiri wa matini mbali na kupotosha

waumini, kuathiri maudhui yaliyomo kwenye matini za kidini na mgongano wa maslahi miongoni mwa waumini.

Katika kufunza mafunzo ya uinjilisti, White alitaja kuwa mwinjilisti anafaa awe kielelezo cha jamii kwa kuwa uongozi na ufanisi wa kanisa unamtegemea. Waumini waliposailiwa kuhusu sifa za mwinjilisti, walitoa matokeo yafuatayo:

Jedwali 9: Sifa za Mwinjilisti

	Utukiaji	%
Uaminifu na kuwa kielelezo cha wengine	36	36
Mwombaji na anayesoma vitabu vya kidini	19	19
Anaeneza ujumbe wa Mungu uadilifu	15	15
Mwenye imani na kuongozwa na roho mtakatifu	3	3.0
Bila majibu	3	3.0
Jumla	23	27.3
	99	100.0

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Jedwali 9 linaonyesha majibu ya waumini kuhusu sifa za mwinjilisti. Kwa jumla (79%), walisema kuwa anafaa kuwa mwaminifu, kielezo, mwombaji, anayeelewa vitabu vya Mungu na kuongozwa na roho mtakatifu. Mwisho, (23 %) ya waumini hawakuwa na jibu lolote. Matokeo hayo yalionyesha kuwa huduma zinazotolewa na wainjilisti kanisani ni muhimu ingawa wengine walionyesha kutoelewa majukumu yao kanisani. Vilevile, uchunguzi ulibaini kuwa, waumini kadhaa wanashindwa kuelewa na kufasiri vitabu tafsiri vya White. Wahubiri walihojiwa kuhusu visababishi vya matatizo ya uelewaji na ufasiri ujumbe wa uinjilisti, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: (14.3%) walisema kuwa waumini hawana muda wa kuvisoma, (28.6%) walitaja mila na desturi baina ya jamii mbili zinazohusika, (28.6%) walisema njia dhaifu za kutafsiri, (14.3%) walitaja ukale wa matukio, na (14.3%) walisema waumini hawathamini lugha ya Kiswahili. Matokeo hayo, hali kadhalika, yanaonyesha kuwa uelewaji na ufasiri wa ujumbe unaathiriwa na ukosefu wa umakini wa usomaji, tofauti za mila na desturi, njia za kutafsiri na ukale wa matukio kama inavyojitokeza katika maelezo hayo.

Mbinu ya Unukuzi

Katika kufunza mafunzo ya uinjilisti, mwandishi asilia alitumia unukuzi wa vifungu mbalimbali kama njia ya kuonyesha mamlaka ya ujumbe anaofundisha kutoka Biblia lakini wakati wa kuhamisha ujumbe huo kutoka matini asilia hadi matini pokezi, mtafsiri alisababisha aina anuwai ya matatizo ya kitafsiri ambayo yanaathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe asilia. Baadhi ya matatizo hayo ni ya kimuundo na kisarufi kama inavyojitokeza katika mfano wa 2 (i na ii) hapa chini. Kwa kufikia malengo yake, White alitumia unukuzi kama vile “Mungu alisema” na “Yesu alinena” kama viashiria vya kuonyesha mamlaka ya ujumbe wake. Aliongezea kuwa, matumizi ya maneno kama vile “nafikiria”, “tunaamini”, “kanisa yetu inafundisha” hayatoi ushahidi wa mamlaka ya ujumbe wenyewe. Matumizi ya maneno hayo ya yanapotafsiriwa kutoka MA hadi MP, inaonekana kuwa ujumbe hahuhamishwi kwa viwango vilivyo sawa. Hali hii ilionyesha kuwa msomaji alipata matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

Mfano wa 2

MA: And the only way to God is Christ. He says, "I am the way, the truth and life; no man cometh unto the Father, but by me." John 14:6, uk. 10

MP: Tena Kristo ndiye njia peke yake ya kumfikia Mungu. Asema, "Ndimi niliye njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba bila kwa mimi." Yoh.14:6. Uk. 11.

Katika mfano wa 2 (i) lengo la mwandishi asilia ni kuonyesha vile mwenye dhambi anavyomhitaji Mungu na njia ya kumfikia ni kupitia Kristo. Ingawa mtafsiri amefaulu katika tafsiri hii, mtafsiri amesababisha matatizo ya kisarufi na kimuundo yanayoathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe. Tazama mfano ufuatao:

MA: No man cometh unto the Father, but by me.

MP: Mtu haji kwa Baba bila kwa mimi.

Katika mfano wa 2 (ii), sentensi *no man cometh unto the Father, but by me* imetafsiriwa kama *Mtu haji kwa Baba bila kwa mimi*. Tafsiri ya sentensi hiyo inafaa kuwa *hakuna mtu ajaye kwa Baba bila kupitia kwake*. Mtafsiri amechanganya nafsi na kwa hiyo, kuathiri viwango vya uelewaji na ufasiri wa ujumbe lengwa. Vilevile, sentensi *And the only way to God is Christ* imetafsiriwa kama *Tena Kristo ndiye njia peke yake ya kumfikia Mungu* badala *Tena njia ya pekee ya kumfikia Mungu ni Kristo*. Katika sentensi hiyo, mtafsiri amebadilisha majukumu ya nomino Kristo na kwa hivyo, kusababisha tatizo la uelewaji na ufasiri wa ujumbe wa mwandishi asilia.

Nida na Taber (1969) wanasema kuwa matini iliyotafsiriwa inapaswa kimsingi na kinadharia kuwa sawa kisemantiki, sahihi kisarufi, usawa wa kimuundo na muumano wa kimatini uliosawa na makala pokezi. Basi kwa kuzingatia maelezo hayo ya Nida na Taber (wametajwa), mtafsiri hakuvizingatia vipengele vyote vilivyotajwa hapo juu katika kuhamisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Matumizi ya Mashairi

Mashairi ni njia mojawapo mwandishi alitumia kufundishia mafunzo ya uinjilisti katika MA. Ushairi ni utungo wa kisanaa wenye mpangilio

maalumu wa lugha ya mkato katika usemi, maandishi au wimbo unaoeleza wazo fulani, hisi au tukio juu ya maisha na ambayo hufuata utaratibu wa urari na muwala maalumu unaoheshimu na kuzingatia kanuni za utunzi wa ushairi unaohusika (Wamitila, 2004). White alidhamiria kutumia mashairi kama njia mojawapo ya kuhubiri injili na kumsifu Mungu. Lakini mtafsiri katika kuuhamisha ujumbe uliojikita katika mashairi hayo, alisababisha matatizo kadha wa kadha ambayo pia yaliathiri uelewaji na ufasiri wa msomaji wa matini pokezi. Tazama mfano:

MA: "The eyes of all wait upon Thee; And Thou givest them their meat in due season.

Thou openest Thine hand, And satisfiest the desire of every living thing." Psalm 145:15, 16.

MP "Macho yao wote yakutazamia wewe; Nawe huwapa chakula chao majira yake. Hufunua mkono wako, Humshibisha kila hai uradhi." Zaburi 145:15,16.

Katika shairi hili (*Njia Salama*, uk1), mtafsiri ametumia mbinu ya moja kwa moja kuhamisha miundo ya LA hadi LP na kwa hiyo, kusababisha matatizo ya kisemantiki na kitamaduni katika shairi hilo. Kwa mfano, neno *meat* tafsiri yake ni *nyama*, lakini katika MP limetafsiriwa kama *chakula* ili kukidhi mahitaji ya hadhira lengwa na tofauti za utamaduni wa jamii inayohusika. Tatizo lingine linajitokeza pale ambapo mtafsiri ameshindwa kubainisha anayefungua mkono. Tazama mfano:

MA: Thou openest Thine hand

MP: Hufunua mkono wako,

Katika mfano wa 2 (iv), mshairi katika MA, anasema anaomba Mungu afungue mkono wake aweze kumbariki lakini katika MP maana ya kitendo hicho imebadilika na Mungu ndiye anayefungua mshairi mkono. Tafsiri sahihi ingekuwa *Hufungua mkono wake*. Licha ya kupoteza maana msingi ya lugha asilia, tafsiri hiyo inapotosha. Larson (1984) anazipinga tafsiri za moja kwa moja akisema:

"Tafsiri za moja kwa moja ni upuuzi na hazina umuhimu wowote katika kuwasilisha ujumbe."

Tafsiri za moja kwa moja husababisha kutoeleweka kwa mtafsiri na pia kudhoofisha ujumbe uliotafsiriwa. Tafsiri dhaifu ya mashairi katika *Njia Salama*, inasababisha kupotea kwa maana, mdundo na ladha ya ushairi kwa jumla na kwa hivyo, kusababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri kwa msomaji.

Mbinu ya kutafsiri neno kwa neno inasababisha matatizo ya ufasiri wa ujumbe. Vilevile njia hii inakuwa mzigo wa kuelewa na kufasiri ujumbe miongoni mwa wasomaji kwa sababu miundo na mipangilio ya maneno katika lugha moja mahususi, hutofautiana katika lugha moja na nyingine.

Mtafiti anatoa hoja kwamba tafsiri ya aina hii huwa tatizo wakati inapotumiwa katika kutafsiri mashairi. Kwa mfano, mwandishi akielezea kuhusu kutubu (uk.12- 22) amenukuu ushairi ufuatao (Zaburi 32:1-2):

MA: “*Blessed is he whose transgression is forgiven, whose sin is covered. Blessed is the man unto whom the Lord Imputeth not iniquity, And in whose spirit there is no guile.*” Psalm 32:1, 2.

MP: “*Heri aliyesamehewa makosa, aliyestirikiwa dhambi, Heri mwanadamu, Bwana asiyemhesabia hatia, Rohoni mwake isipokuwa hila.*” Zaburi 32:1, 2.

Jedwali 10: Ulinganifu wa Visawe

MA	MP
Sorrow	Hali mbaya
Misery	Dhambi
Comfort	Kutuliza roho zetu
There are flowers upon the thistles, and the thorns	Kila m ti wa miiba una maua yake
The world, though fallen,	Ingawa dunia imeanguka
In nature itself are messages of hope	Lakini yote yaliyomo yana matumaini

Chanzo: (Data ya nyanjani, 2019)

Katika Jedwali 10, mtafsiri amehamisha maneno kwa kutumia njia ya moja kwa moja. Kwa mfano, neno *sorrow* katika makala chanzi, limetafsiriwa kama *hali mbaya*. Neno hili lina visawe vyake vya kutosha katika lugha ya Kiswahili lakini mtafsiri amelitafsiri kama *hali mbaya*. Tafsiri sahihi katika Kiswahili sanifu ni *huzuni*, *masikitiko*, *majonzi*, *majuto* na *simanzi*. Pili, neno *misery* katika MA, limetafsiriwa kama *dhambi*. Tafsiri sahihi ingekuwa

Katika mfano wa 2 (v), mtafsiri amebadilisha mpangilio wa maneno katika lugha pokezi. Mathalan, mpangilio wa sentensi *Blessed is he whose transgression is forgiven, whose sin is covered* imetafsiriwa kama *Heri aliyesamehewa makosa, aliyestirikiwa dhambi*. Katika tafsiri hiyo, neno *baraka* limeondolewa na kwa hivyo kuathiri ujumbe wa matini tafsiri. Vilevile, sentensi *And in whose spirit there is no guile* mtafsiri ameondoa kiunganisha *and* katika mshororo pokezi na kwa hivyo, kuathiri maana ya mshororo *Rohoni mwake isipokuwa hila*.

Tatizo linalojitokeza katika kuyaelewa na kuyatafsiri mashairi, ni ukosefu wa utaratibu maalumu, udumishaji wa sifa za kikaida za ushairi kama vile mikazo, ridhimu, ucheshi, kinaya au kubadilisha ploti moja hadi nyingine katika matini. Kwa hivyo, mtafsiri anahitaji kibali cha ushairi ili aweza kuhamisha ujumbe kikamilifu kutoka makala asilia hadi makala pokezi.

Tatizo lingine linalojitokeza katika kutafsiri mafunzo ya White katika matini teule ni tafsiri ya moja kwa moja. Katika hali hii mtafsiri anapohamisha maana ya maneno kutoka MA hadi LP, kwa njia ya moja kwa moja, hadhira lengwa inakumbana na matatizo ya kuelewa na kufasiri maana msingi (MA) na maana rejelewa katika MP. Tazama Jedwali lifuatalo:

taabu, *shida* au *mashaka*. Tatu, neno *Comfort* lina visawe vyake katika lugha pokezi kama vile *fariji*, *faraja*, *liwaza*, *burudisho* na *fanaka*. Lakini mtafsiri aliamua kutumia maelezo kama *kutuliza hali zetu*. Ingawa maelezo haya ni sahihi, msomaji hawezi kuelewa ni kwa misingi gani anaweza kutuliza hali yake. Kwa hivyo, tafsiri sahihi ingekuwa kama ifuatavyo:

MA: There are flowers upon the thistles, and the thorns are covered with roses.

MP: Kuna maua juu ya magugu, na miiba imefunikwa na maua ya waridi.

MA: In nature itself are messages of hope and comfort.

MP: Kwenye asili yenyewe kuna ujumbe wa matumaini na faraja.

Hali kadhalika, *Jedwali 8*, mtafsiri amekosa visawe vinavyolingana na maneno katika lugha pokezi. Hali hiyo ilimfanya kudondosha baadhi ya maneno, vishazi, virai na basi kutofaulu kuwasiliana na hadhira yake. Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa mtafsiri amehamisha ujumbe bila kuzingatia tofauti za kiekolojia na miktadha baina ya LA na LP. Kwa hivyo, hakutilia maanani *skopos* ya wasomaji lengwa. Kwa mfano, maneno *thistles* na *thorns* yana maana tofauti katika MA lakini katika LP mtafsiri ameyahamisha kama maneno yenye maana moja sawa, *Miiba* na kwa hiyo, kupoteza maana msingi ML.

Jambo lingine linaathiri mafunzo ya injili linatokana na mbinu za kufundisha. Katika kufanikisha mafundisho, White katika *Njia Salama* amependekeza baadhi ya mbinu za kueneza na kufundisha injili. Kwa mfano, akifundisha kuhusu majaribu ya kuwa mfuasi wa Yesu, (uk. 42-51), aliwashauri wanasabato wabadilishe tabia na mienendo yao, wawe na uhusiano mwema na heshima yao ya kibinafsi miongoni mwa nyingine. Lakini, mafunzo hayo yalieleweka na kufasiriwa kwa njia tofauti na wanasabato. Tazama mfano wa ufuatao:

MA: A change will be seen in the character, the habits, and the pursuits. The contrast will be clear and decided between what they have been and what they are. The character is revealed, not by occasional good deeds and occasional misdeeds, but by the tendency of the habitual words and acts.

MP: Itaonekana kwamba tabia zetu, desturi zetu, mazoezo yetu, na mambo yetu yote yamegeuka kuwa mbalimbali na yale ya zamani. Tabia na desturi za mtu Fulani zinajulikana si kwa matendo mema au mabaya

ya siku moja moja tu, ila kwa maelekezo ya matendo yake na maneno yake, na mazoezo yake ya siku zote.

Katika mfano wa 2 (vii), ingawa mwandishi anawasilisha ujumbe asilia kwa kuzingatia lengo lake, mtafsiri amehawilisha kwa njia tatanishi. Kwa mfano, sentensi *Itaonekana kwamba tabia zetu, desturi zetu, mazoezo yetu, na mambo yetu yote yamegeuka kuwa mbalimbali na yale ya zamani*. Inafaa kutafsiriwa kama: *Badiliko litaonekana katika tabia, mazoea na shughuli zetu*. Kwa hivyo, katika tafsiri hiyo, dhana ya badiliko haijaitokeza vilivyo katika MP. Pengo hilo, linamnyima msomaji uelewa na ufasiri wa funzo la mwandishi asilia. Vilevile tazama sentensi zifautazo:

MA: The contrast will be clear and decided between what they have been and what they are.

MA: Kinyume cha hayo itakuwa wazi na kuamuliliwa vile walivyokuwa na vile walivyo sasa.

Katika mfano wa 2(viii), makala asilia yamewasilishwa kwa njia ya kueleweka lakini MP inakanganya msomaji kwa namna mbalimbali. Kwanza, kishazi *The contrast will be clear* kimetafsiriwa kama *Kinyume cha hayo itakuwa wazi* badala ya *kinyume chake kitakuwa wazi*. Pili, kishazi *decided between what they have been and what they are* kimetafsiriwa kama *na kuamuliliwa vile walivyokuwa na vile walivyo sasa* badala ya *kuamuliwa vile vilivyokuwa awali na sasa*. Tafsiri za vishazi hivyo viwili zina makosa ya kisemantiki ambayo yanasababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri.

Makosa ya kisemantiki, yanasababisha tafsiri finyu au pana ya matini asilia. Tafsiri finyu au pana inaweza kuathiri sehemu ya maana au kupotea kwa maana yote katika makala tafsiri. Hali hii inajitokeza katika matini tafsiri za kidini, kutokana na ukosefu wa usawa wa ulinganifu wa maana tofauti za miundo baina ya lugha mbili zinazohusika.

Mbinu ya Mahojiano

White alitumia mbinu ya mahojiano kufundishia. Ingawa alifaulu kutimiza malengo yake, mbinu hii

inasababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe tafsiri kwa msomaji lengwa. Tazama mifano:

MA: Jesus: He answered and said unto him, verily, verily, I say unto thee, except a man be born again, he cannot see the kingdom of God.

MP: Yesu: Akamwambia, “Kweli nakwambia, mtu asipozaliwa upya hataweza kuuona ufalme wa Mungu.”

Katika mfano wa 2 (ix) ujumbe katika MA ulielezwa kwa njia iliyo wazi lakini uhawilishaji wa MP ulimtatiza msomaji kwa namna mbalimbali. Kwanza, kishazi *He answered and said unto him* kinatatiza kwa sababu kimetafsiriwa kama *akamwambia* badala ya *akamjibu na akamwambia*. Katika uhamishwaji huo, neno *akamjibu* limeondolewa na kwa hivyo, kusababisha pengo la maana. Pili, kirai *verily, verily* kimetafsiriwa kama *kweli* badala ya *hakika, hakika*. Tatu, semi *cannot to see* imetafsiriwa kama *hataweza kuuona*. Usemi huo una maana msingi na maana rejelewa ambayo inaweza kumtatiza msomaji. Kwa kuzingatia muktadha, msemaji alimaanisha kwamba mtu hawezi kuurithi ufalme wa mbinguni. Tazama mfano:

MA: Nicodemus: He saith unto him, How can a man be born when he is old? Can he Enter the second time into his mother's womb, and be born?

MP: Nikodemo: Akamwuliza, “Mtu mzima awezaje kuzaliwa tena? Hawezi kuingia tumboni mwa mama yake na kuzaliwa mara ya pili!”

Hali kadhalika, ujumbe katika mfano wa 2 (x), MA ulielezwa kwa njia ya wazi lakini MP ilihawilishwa kwa njia tatanishi. Kwa mfano, kirai *He saith unto him* kimeachwa nje katika MP. Vilevile, swali *Can he enters the second time into his mother's womb, and be born?* Limetafsiri kwa nja ya moja kwa moja bila kuzingatia maana msingi. Mtu hawezi kurudishwa kwenye tumbo la mama yake na kuzaliwa upya lakini maana inayojitokeza ni kuwa lazima mkristo azaliwe kwa roho ili aurithi ufalme wa mbinguni. Kwa hivyo, lugha ya mafumbo, udondoshaji na kutozingatia miktadha katika tafsiri

ya mahojiano, iliathiri uelewaji na ufasiri wa ujumbe kwa msomaji.

Matumizi ya Methali

Katika kufundisha mafunzo ya uinjilisti White alitumia methali. Lakini katika kutafsiri methali hiyo, mtafsiri alisababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa ujumbe ambayo yaliathiri msomaji lengwa. Tazama mifano:

MA: ---You catch more flies with honey than with vinegar (pg 47).

MP: --- Unashika nzi wengi kwa kutumia asali kuliko kwa kutumia siki (uk 57).

Katika mfano wa 2(xi) methali *You catch more flies with honey than with vinegar* imehamishwa kama *Unashika nzi wengi kwa kutumia asali kuliko kwa kutumia siki*. Mtafsiri aliitafsiri kwa njia sisisi. Mfano wa (xi) unaonyesha namna tafsiri sisisi inayvofanyika, licha ya kuzingatia muundo wa lugha lengwa lakini pia mbinu hii ina udhaifu wake kwamba haizingatii muktadha na wakati mwingine hutoa tafsiri yake hupotosha ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, mwandishi asilia aliwashauri wahubiri kutumia njia ya upendo kuwashawishi waasi kubadilisha nyendo zao na kumkubali Yesu. Tafsiri hiyo huwa na uchangamani hasa kwa msomaji asiyeafahamu tofauti za utamaduni baina ya Kiingereza na Kiswahili.

Tazama mfano mwingine:

MA: The sinners “shall be holden with the cords of his sins.” (Proverbs 5:22).

MP: “Maovu yake yatamkamata mwovu mwenyewe, naye atashikwa kwa kamba ya dhambi yake (Methali 5:22).

Katika mfano wa 2 (xii), methali *The sinners “shall be holden with the cords of his sins.”* Imetafsiriwa kama *Maovu yake yatamkamata mwovu mwenyewe, naye atashikwa kwa kamba ya dhambi yake*. Methali tafsiri imetafsiriwa kwa njia ya unukuzi yaani ujumbe ule ule umelezwa kwa kutumia maneno mengine. Ingawa mtafsiri amefanikiwa kuhamisha ujumbe wa kuonya mwenye dhambi, alisababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa habari. Kwa mfano, neno *sin* limetafsiriwa kama *maovu, the sinners*

limetafsiriwa kwa umoja kama mwovu. Matatizo hayo yanaondoa uasilia na uaminifu katika matini na kwa hiyo kuwanyima wasomaji uelewa wa habari msingi. Methali hii inalenga Inaonya kuwa mwenye makosa atafungwa na makosa yake. Kadhalika, inalenga kutoa onyo na kuonyesha madhara yanayotokana na kutenda dhambi. Basi, ujumbe wa methali unafaa kuhamishwa kwa kuzingia umakini na muundo asilia ili kudumisha lengo la mwandishi asilia.

Methali nyingine ambayo inatekeleza malengo ya kuonya, kukosoa na kushauri imenukuliwa kutoka kitabu cha Methali (28:13) katika matini ya *Njia Salama*. Tazama mfano wa ufuatao:

MA: He that covers his sins shall not prosper; but whoso confesseth and forsaken them shall have mercy (Proverbs 28: 13).

MP: “Mwenye kusetiri makosa yake hatasitawi: kila aziungamaye na kuziacha atarehemiwa.” (Methali 28:13). Methali ya mfano wa 2 (xiii) pia inatekeleza majukumu ya kidini. Inamwonya mtu dhidi ya kusetiri dhambi kwani hatastawi. Inafaa akiri na kuziungama dhambi ili aweze kurehemiwa. Methali hii vilevile, inalenga kuwaonya watu wanaobania makosa yao ili wasifanye toba. Hata hivyo, ujumbe huo ulihamishwa kwa njia ya kutatanisha. Kwa mfano, muundo wa methali umebadilishwa kwa sababu mtafsiri ameuwasilisha kwa njia ya taarifa badala kuzingatia muundo wa methali asilia. Ukiushi huu ulisababisha matatizo ya uelewaji na ufasiri wa msomaji. Kwa mfano, msomaji anakumbana na changamoto anaposoma matini zinazosheheni methali kama wasifu wa kimsingi wa usanifu wake, inayohusiana na ukweli kwamba methali ni kauli dumifu zisizobadilika kwa urahisi (Ghazala, 1995). Vilevile, uibushaji wa maana iliyokitwa katika methali unaweza kuwa jambo telezi au hata gumu lisilowezekana wakati maana inayotafsiriwa imekitwa katika methali iliyo na mshikamano wa karibu sana na tamaduni zinazomochipuka. Hali kadhalika, kutafsiri methali katika matini za kidini ni uhalisi unaobainika katika hali changamano ambamo mtafsiri anakuta kwamba methali husika haiwezi kutafsiriwa nje ya miktadha ilimotumiwa wala kupuuza uamili uliokusudiwa kutekelezwa na methali hiyo katika miktadha hiyo. Basi, tafsiri zozote za methali zinazopuuza uhalisi huu zinaweza kuibua matatizo ya uelewaji na ufasiri

wa aina mbalimbali yanayoweza kuishia kupotosha maana na mawasiliano, udhoofishaji wa usanifu wa matini lengwa.

HITIMISHO

Vipengele vya kiisimu, kimtindo, kimuundo, kitamaduni na kimuktadha ni muhimu katika kutafsiri matini za Kiingereza hadi Kiswahili. vipashio hivyo vikipuuzwa, msomaji atashindwa kupata maana msingi iliamishwa. Hii ina maana kwamba matini asilia haitakuwa na maana kwa wasomaji kwani ujumbe zalishi utakuwa tofauti. Kwa hivyo, mtafsiri anafaa kuzingatia tofauti za kiisimu na kitamaduni za lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili aweze, kufanikiwa kuhamisha ujumbe msingi kutoka lugha asilia hadi lugha pokezi kwa ustadi.

MAREJELEO

- Anna, Matamala. (2009). *Terminological Challenges in the Translation of Science Documentaries: A Case Study, Across Languages and Cultures*,11(2):255-272.
- Chaula, N. (2012). *Insufficiency Translation In Religious Texts Its Causes, Effects and Solutions*. LAP Lambert Academic Publishing
- Eugene, A. Nida. & Charles, Taber. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Laiden. Brill Publishers.
- Ghazala, Hasan. (1995). *Translation as problems and solutions*. (10th ed.). Jeddah: Konooz Elmarefa.
- George, R. Knight. (2009). *A search for identity: The development of Seventh-day Adventist beliefs*. Hagerstown, MD: Review and Herald.
- Jeremy, Munday. (2008). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. Leiden. Routledge.
- Jeremy, Munday. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. Leiden. Routledge.
- Joel, Donald, Heck. (2011). *Evangelism*. Blackwell.Blackwell Publishing Ltd.

- John, Hedley, Brooke. (2011). *Science and Religion Around the World*, (eds). New York: Oxford University Press.
- John, Touliatos & Compton, H., Norma. (1988). *Research methods in human ecology/home economics*. Ames, Iowa: Iowa State University Press.
- Kombo K.D., & Tromp, L.,A.,D., (2006). *Proposal and Thesis writing: An introduction*. Nairobi. Paulines Publishers.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. 2nd Revised. New Delhi: New Age International.
- Knight, R., George. (2009). *A search for identity: The development of Seventh-day Adventist beliefs*. Hagerstown, MD: Review and Herald.
- Malangwa, S., Pendo. (2017). *The Significance of Cross-Fertilization Practices in Kiswahili technical and Specilized Translation*, The Journal for Studies in Humanities and Social Sciences, 6(1):154-169.
- Mike, Mazzalongo. (2019). *The Idea of A Christian*. University Essays in Theology And Higher Education.
- Lawrence, B., Venuti. (2008). *The translator's invisibility: A history of translation*. USA. Routledge.
- Reiss, Katharina (1990). *Towards of General theory of translation action*. Skopos Theory Explained. London &New York. Routledge.
- Reiss, Ktharina &Vermeer, J., Hans (1984). *Groundwork for a General Theory of Translation*. Neimeyer. Tubergen.
- Schaffner, C. (1998). *Action (Theory of Translational action)*. In M. Baker, ed. Routledge Encyclopedia of Translation Studies. London: Routledge, pp 3-5.
- Vermeer, Hans. (1989). *Skopos and translation Commission*. Heidelberg: Universitat.
- Vermeer,J., Hans. (1978) *Ein Rahmen Fur eine allgemeine translationsthe Sprachen*, London &New York. 23. 95-98.
- Wamitila, Kyalo, Wadi. (2004). *Kamusi ya tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishangao*. Lulu za Lugha 3. Nairobi. Longhorn publishers.
- Wang, Mian. (2012). *International Conference on Education Technology and Management*. Engineering Lecture Notes in Information Technology, Vols.16-17